**Mradi Na. 4280: MRADI WA TANZANIA YA KIDIGITALI (*DIGITAL TANZANIA*)**

Katika mwaka 2022/23 **Sh. 39,300,000,000** fedha za nje ziliombwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali. Katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 vipaumbele vilivyoainishwa kwenye mradi huu ni:

(i) Kujenga kituo kimoja (1) cha kukuza taaluma na ubunifu katika TEHAMA na vituo vidogo vitano (5) kwenye kila Kanda;
(ii) Kuwezesha ununuzi, ugavi na ufungaji wa vifaa katika kituo kimoja (1) kikubwa na vituo vidogo vitano (5) vya kukuza taaluma na ubunifu katika TEHAMA;
(iii) Kuwezesha ununuzi wa 'bandwidth' kwa ajili ya matumizi ya intaneti ya Serikali;
(iv) Kusimika mitambo kwa ajili ya kuboresha Kituo cha Taifa cha Kutunzia Data (NIDC);
(v) Kukarabati vituo 10 vya Huduma Pamoja;
(vi) Kujenga mfumo wa kitaifa utakaorahisisha ukusanyaji wa takwimu za masuala ya TEHAMA;
(vii) Kujenga, kupanua na kuboresha miundombinu iliyopo ya intaneti yenye kasi (broadband) inayomilikiwa na Serikali (GovNET) na kuunganisha taasisi 100 kwenye Miundombinu hiyo na kufikisha taasisi 390 zilizounganishwa;
(viii) Kutekeleza programu ya uelimishaji umma kuhusu mradi;
(ix) Kujenga maabara tatu (3) kwa ajili ya kufufua (refurbishment) vifaa vya TEHAMA katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza;
(x) Kujenga minara ya mawasiliano 150 kwenye Kata 150 ili kuwezesha huduma za mawasiliano nchini;
(xi) Kufanya mapitio na kuhuisha Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali za TEHAMA;
(xii) Kuwajengea uwezo wataalam wa TEHAMA nchini kwa kuwapatia watalaam 200 mafunzo ya muda mfupi na wataalam 10 mafunzo ya muda mrefu; na
(xiii) Kufanya tathmini ya kuainisha mahitaji na usanifu wa kujenga mfumo wa kuwezesha biashara mtandao.

Hadi kufikia **tarehe 31 Disemba, 2022** Wizara ilipokea jumla ya kiasi cha Sh. **10,261,846,606.50** sawa na asilimia 26.11% ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Mradi tajwa. Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi husika ni kama ifuatavyo:

(i) Kufanyika maandalizi ya kupata mtaalam kwa ajili ya upembuzi yakinifu kuhusu Kuanzishwa kwa Taasisi ya TEHAMA na vituo vya Ubunifu wa TEHAMA. Mkataba kati ya Wizara na Mshauri Mwelekezi umesainiwa mwezi Disemba, 2022 na kazi hiyo itakamilika mwezi Aprili, 2023;
(ii) Kuhakiki taarifa za anuani za makazi katika Halmashauri **11** ambazo ni Majiji ya Dar es salaam na Mwanza, Manispaa za Ilemela, Ubungo, Temeke, Kinondoni, Kigamboni na Mtwara Mikindani, Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Micheweni na Chakechake;

(iii) Kufanyika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya kufanya mapitio ya sera na sheria zinazosimamia TEHAMA. Taarifa ya awali (Final Inception Report) imewasilishwa na Mshauri Mwelekezi na kazi hiyo inarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2023.

(iv) Kufanyika kwa Upembuzi yakinifu kuhusu Utengenezaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taarifa za Takwimu za TEHAMA (NISMIS). Mkataba kati ya Wizara na Mshauri Mwelekezi umesainiwa Novemba, 2022 na ameanza kazi ya kukusanya maoni ya wadau kabla ya kuanza kusanifu mfumo huo, utekelezaji wake utakamilka mwezi Mei, 2023.

(v) Kukamilisha Mpango Mkakati wa Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taarifa za Takwimu za TEHAMA (NISMIS) na orodha ya viashiria vya TEHAMA.

(vi) Kuhuisha ununuzi wa Mkondo wa Mawasiliano ya Serikali (Extension of Government Internet Bandwidith) wenye kasi ya 5GBps kwa kipindi kinchoishia mwezi Februari, 2023 kwa ajili kuongeza ubora wa upatikanaji wa huduma za Kidijitali zinazotolewaa na Serikali. Aidha, taratibu za manunuzi ya Mkondo wa Mawasiliano ya Serikali wenye kasi ya 20 GBps kwa kipindi cha miaka kumi ijayo upo katika hatua ya tathmini ya zabuni na Mkataba unatarajiwa kusainiwa mwezi Februari, 2023.

(vii) Kufanyika kwa upembuzi yakinifu wa Teknolojia ya (TV White Space) itakayosaidia kuongeza huduma ya mawasiliano kwa watumiaji wa intaneti kwenye maeneo ya vijijini na pembezoni mwa Nchi. Mshauri Mwelekezi amewasilisha taarifa ya awali ya upembuzi na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2023.

(viii) Kukamilika kwa taratibu za Manunuzi ya vifaa kwa ajili ya upanuzi wa Mkondo wa Mawasiliano ya Serikali (Bandwidith termination Equipment). Vifaa hivyo vinatarajiwa kupokelewa mwezi Juni, 2023 na kuboresha uwezo wa Mkondo wa Mawasiliano ya Serikali.

(ix) Kuandaa daftari la huduma za Serikali kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma za Serikali kwa wananchi (Government Service Directory).

(x) Kutangaza ufadhili wa nafasi za masomo kwa watumishi wa Serikali wa kada ya TEHAMA kwa ngazi ya Shahada ya Uzamili. Uchambuzi wa watumishi watakaofadhiliwa katika mafunzo hayo unatarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi Januari, 2023 na matokeo kutangazwa baada ya kukamilika kwa zoezi hilo. Watumishi wanatarajiwa kaanza masomo mwishoni mwa Mwezi Februari, 2023;

(xi) Kufanyika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya vituo vya huduma Pamoja utakaosaidia kurahisisha utendaji kazi wa vituo hivyo (Business Process re-engeering). Taarifa ya awali (Final Inception Report) imewasilishwa. Kazi hiyo inarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2023.

(xii) Kufanya maandalizi ya mpango mkakati wa uchumi wa Kidigitali (Digital Economy Framework 2023-2033) utakaosaidia kuongeza matumizi ya kidijitali kwa huduma zinazotolewa na Serikali pamoja na Sekta binafsi. Rasimu ya mkakati huo inatarajiwa kujadiliwa kweye kikao cha Kamati Kuu Tendaji ya Taifa mwezi Januari, 2023.